MWONGOZO WA JUKWAA LA KIULIMWENGU LA USALAMA WA

eisf

JUKWAA LA USALAMA WA MASHIRIKA YA ULAYA

# Kudhibiti Ukatili wa Kijinsiadhidi ya Wafanyakazi wa Misaada:

## kuzuia, utayari, kukabiliana na baada ya utunzaji

Dondoo

*Kazi ya sasa ni tafsiri isiyo rasmi ambayo mchapishaji anakubali jukumu kamili. Chapisho hili lilitafsiriwa kwa uhuru na mashirika yafuatayo: Shirika la Social Development Direct na Translators without Borders.*

# 1 Kuzuia




*'Ukatili wa kijinsia kwa ujumla unahusu mamlaka, siyo ngono.'*

Jitihada za kuzuia na utayari zinalenga kupunguza uwezekano wa visa vya ukatili wa kijinsia kutokea. Ili kuzuia ukatili wa kijinsiadhidi ya wafanyakazi wa misaada, ni muhimu pia kulenga kuwakataza wahalifu wanaoweza kujitokeza na kushughulikia udhaifu na hatari kwa ukali.

## 1.1. Kuelewa hatari

Baadhi ya mifumo ya kuzuia inalenga sana kudhibiti mwenendo wa wafanyakazi kama njia ya kuzuia ukatili wa kijinsia. Mitazamo kama hiyo inatoa wito kwa wafanyakazi – hasa wanawake – kuepuka kuvaa mavazi ya kufunua na kunywa pombe, miongoni mwa tabia zingine. Aina hii ya mitazamo ya kuzuia inachukulia kwamba manusura wangeweza kuzuia ukatili wa kijinsia ikiwa angeenenda kwa namna tofauti.

Mitazamo inayolenga kudhibiti mwenendo wa wafanyakazi inaweza kuendeleza desturi ya kulaumu muathiriwa na kujenga mazingira ya shirika ambapo ukatili wa kijinsia unaonekana kama inaruhusiwa katika hali fulani.

Mitazamo ya kuzuia inapaswa kulenga katika kuzuia wahalifu na kupunguza udhaifu na masuala ya hatari kwa ukali na ukatili wa kijinsia.

Zaidi ya hayo, juhudi zote za kuzuia zinahitaji kuwa na mtazamo wa usawa kwa mtu binafsi pamoja na udhaifu wa nje na wa shirika na masuala ya hatari (kama vile mazingira ya shirika yanayoruhusu visa hivi).

### 1.1.1. Wahalifu ni akina nani?

Ripoti ya Kituo cha Kimataifa cha Feinstein 'Komesha Shambulio la Kingono Dhidi ya Wafanyakazi wa Misaada ya Kibinadamu na Maendeleo' inaonyesha kuwa idadi kubwa ya wahalifu wa ukatili wa kijinsia dhidi ya wafanyakazi wa misaada ni wanaume wanaofanya kazi katika sekta ya misaada au wanaume walioajiriwa na mashirika ya misaada kama walinzi.
Wahalifu wanaweza pia kutoka kwa vikosi vyenye silaha, vikundi vyenye silaha au jamii ya eneo ambalo wafanyakazi wa misaada wanafanya kazi. Visa vya ukatili wa kijinsia vilivyoripotiwa kwa Shirika lisilo la Kiserikali la Report the Abuse na kuwasilisha katika ripoti yao 'Uzoefu wa Kibinadamu wa Ukatili wa Kijinsia' inaonyesha kuwa asilimia 92 ya wahalifu wa ukatili wa kijinsia dhidi ya wafanyakazi wa misaada walikuwa wa kiume. Kutokana na kuripotiwa kwa visa kama hivyo, asilimia hizi huenda hazitoi picha kamili ya uwiano halisi wa kijinsia wa wahalifu.

## Kukabiliana na habari potofu

- 'Hatari ya mgeni' kwa kawaida huchukuliwa kama hatari kubwa zaidi ingawa kuna uwezekano mkubwa kuwa mhalifu ni mtu ambaye mnusura anamfahamu.
- Visa vya ukatili wa kijinsia sivyo vitendo vya vurugu sana kila wakati na vinaweza kutofautiana kwa kiasi kikubwa.
- Ingawa wanawake wana uwezekano mkubwa wa kulengwa, wanaume wanaweza kulengwa pia; hali fulani, ikiwemo sifa za kibinafsi na muktadha wa eneo, zinaweza kuzidisha hatari kwa wanaume

Wahalifu wana sababu tofauti za kufanya vitendo vya ukatili wa kijinsia na kufanya ukali kwa njia tofauti. Wanashawishiwa na mchanganyiko wa masuala, kama vile historia yao ya maendeleo na familia, utu, na masuala ya kimazingira na kijamii. Baada ya kushiriki katika ukatili wa kijinsia, wahalifu binafsi huonyesha kuathirika kwa namna tofauti.

Utafiti kuhusu sifa za wahalifu wa ukatili wa kijinsia ni mfinyu. Hata hivyo, utafiti uliofanywa na Kampuni ya RAND kuhusu wahalifu wa kiume wa ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake unaonyesha baadhi ya sifa muhimu:

- unyanyasaji wa utotoni;
- tabia ya ngono yenye hatari kubwa, kama vile historia ya kushiriki

ngono ya kiholela au ngono kwa ajili ya raha tu mahusiano, wapenzi wengi wa ngono, uhalifu wa zamani wa unyanyasaji wa kijinsia;

- stadi changa za mahusiano kati ya watu, kama vile ukosefu wa huruma au ugumu wa kuunda mahusiano;
- mtazamo mkali na utambuzi, kama vile uhasama kwa wanawake, kukubalika kwa habari potofu za ubakaji au ubabedume;
- kushirikiana na wanarika wenye ukatili wa kijinsia, ambayo inaweza kuzidisha hatari kwamba watajihusisha na uhalifu wa kingono; na
- matumizi dawa za kulevya, kama vile matumizi ya wastani au kupindukia ya pombe au dawa za kulevya, ambayo yanaweza kuleta hatari inayohusiana na ukatili wa kijinsia, kwani inaweza kuzuia ufahamu bora (yaani, michakato ya utambuzi ambayo ni muhimu kwa udhibiti wa tabia).

### 1.1.2. Masuala ya hatari ya mtu binafsi kwa ukali

Watu binafsi wanaweza kuchukua hatua za kujaribu kupunguza hatari ya kulengwa na mhalifu kwa kuelewa na kufuata hatua za kukabiliana na hatari za usalama wa kishirika.

**Kwa bahati mbaya, wakati mwingine hakuna kitu mtu anayeweza kufanya ilikupunguza hatari ya kulengwa.**

Wafanyakazi wanapaswa kufahamu kikamilifu kwamba ukatili wa kijinsia ni hatari na kwamba wanaweza kuwekwa hatarini na kwamba kila mtu ana sifa binafsi ambazo zinaathiri hatari yao ya kuwa lengo la ukatili wa kijinsia. Kama ilivyotajwa katika
utangulizi wa mwongozo huu, mwingiliano baina ya utambulisho wa mtu binafsi (mtu mwenyewe), tabia, eneo, wajibu na shirika litajumuishwa katika udhaifu wao binafsi na hatari.

Masuala yanayoweza kuathiri hatari ya mtu kupitia ukatili wa kijinsia yanajumuisha:

- **umri:** umri wa miaka 18–25 una uwezekano mkubwa wa kulengwa kuliko wale wa zaidi ya 50.
- **jinsia:** wanawake wana uwezekano mkubwa wa kulengwa kuliko wanaume.
- **mtazamo wa utaifa na utamaduni:** ubaguzi fulani wa kiutamaduni unaweza kuathiri ikiwa mtu anaweza kulengwa.
- **sifa binafsi:** mitazamo na imani ya utambulisho inaweza kusababisha watu wenye wasifu fulani kulengwa, kama vile wakichukuliwa kama wasagaji, mashoga, jinsia mbili, jinsia tata, mabasha na jinsia changamani (LGBTQI).
- **uwezo:** mtazamo wa uwezo wa mtu kuwa na ulemavu unaweza kuathiri hatari

yao binafsi. Ubaguzi kwa msingi wa uwezo - ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu - pia unaweza kuchangia watu kulengwa.

- **muonekano: watu ambao wanaooneka wazi kuwa tofauti na jamii ya eneo unaweza kuangazia na kuwa katika hatari kubwa kwa sababu hiyo.**
- **pombe:** matumizi ya kupindukia yanaweza kudhuru maamuzi ya watu na kuwafanya waonekane kama malengo rahisi, ambayo yanaweza kuvuta tahadhari ya ngono.
- **tabia ya kuchukua hatari:** kuchukua hatari kunaweza kumfanya mtu aonekane kama lengo rahisi na kuvuta makini ya wahalifu wa kingono.
- **upatikanaji:** wahalifu wanahitaji upatikanaji wa watu binafsi ili kuwaweka katika hali ya hatari, ama kwa kuwafuata nyumbani au kuwapa dawa za kulevya (inayojulikana kama dawa za kulevya za ubakaji) ili kuwaondolea uwezo wao. Ufikiaji huo ni mgumu zaidi kupunguza ikiwa mhalifu ni mwenzake au mtu anayejulikana kwa mtu anayelengwa.
- **ukubwa wa kikundi: watu walio** kivyao au katika jozi wana uwezekano mkubwa wa kulengwa kuliko makundi makubwa.
- **mipaka ya binafsi:** ukosefu wa mipaka ya kitaaluma au wazi unaweza kusababisha visa. Ni muhimu kusaidia wafanyakazi kuhusu njia za kuweka mipaka na kuelewa mipaka ya watu wengine, hasa katika miktadha ya tamaduni mbalimbali.
- **kuruhusu kero ndogo kwenda bila kuripoti: masuala madogo yanayohusisha watu wanaojulikana yanaweza kuongezeka ikiwa hayatashughulikiwa au kuripotiwa.** Ukosefu wa kutoa ripoti unaweza kuzidisha hatari ya kulengwa kwa ukatili wa kijinsia.

Haya ni masuala ya hatari ya kibinafsi yanayowezekana, ambayo yanapaswa kuwasilishwa kwa wafanyakazi na kuzingatiwa katika michakato ya usimamizi wa hatari za usalama wa shirika. Hata hivyo, hata kupunguza hatari hizi hakuhakikishi kuwa mtu ataweza kuepuka kisa.

### 1.1.3. Masuala ya hatari ya nje na ndani hatari ya shirika

Masuala ya hatari kwa ukali hutegemea mazingira wezeshi yanayoruhusumhalifu kutenda uhalifu huo bila kuogopa matokeo. Masualahaya yanaweza kuainishwa kama za nje na za ndani ya shirika.

*'Kanuni za kijamii mara nyingi huwa na nguvu zaidi kuliko utu wa mtu katika kutabiri tabia. Fikiria kuhusu kuhudhuria mechi ya kandanda kwa mara ya kwanza na mashabiki wakishangilia goli linapofungwa – wanasimama na kupiga kelele na kupunga mikono yao. Ikiwa hujawahi kuhudhuria mechi ya kandanda na labda ni mtu wa utulivu, bado unaweza kusimama na kushangilia. Huutarajiwi kukaa kimya na kutazama, unavyoweza kuwa kwenye mechi ya tenisi. Hii ni desturi ya kijamii, na hata kama hufurahii*

*mpira wa kandanda, kuna shinikizo la kijamii kufuata desturi.'*

Huku masuala ya nje kwa kawaida huwa zaidi ya udhibiti wa taasisi moja yoyote, shirika linaweza kuhakikisha kuwa masuala kama hayo hayaamui muundo wake wa ndani, mifumo, michakato au desturi. Muundo na utamaduni wa shirika unapaswa kutambua na kuzingatia (ikijumuisha kukabili, ikiwezekana) desturi za kijamii zisizofaa au zinazoweza kudhoofisha, kama vile:

- mazingira ya uhasama wa kijinsia;
- viwango vya juu vya ukali wa kijinsia;
- uvumilivu wa mahakama ya unyanyasaji wa kijinsia au upendeleo kwa wahalifu;
- taifa lililoshindwa au kuanguka;
- kuvunjika kwa sheria na utaratibu;
- jamii inayotawaliwa na wanajeshi; na
- jamii ya mfumo wa ubadedume au uhafidhina.

Ndani ya shirika, masuala ya hatari ni yale yanayohusiana na muundo wa shirika, michakato na mifumo, ikijumuisha utamaduni wa shirika.
Mazingira na desturi ya shirika yanaweza kuwa na athari kubwa kwa tabia za wafanyakazi. Kwa mfano, ikiwa kanuni za kijamii za shirika zinahusisha kuwatazama wanawake kama vifaa au kutowaheshimu wadogo, wafanyakazi wana uwezekano mkubwa wa kukabiliana na desturi hii kwa tabia ipasavyo.

Shirika linapaswa kulenga kuzuia au kukabiliana na hatari za ndani ambazo zinahusiana na muundo wake, michakato au mifumo yake, ikijumuisha:

- sera dhaifu ya shirika na maandalizi kuhusu ukatili wa kijinsia;
- michakato na taratibu zisizoeleweka za kupiga ripoti;
- utekelezaji duni, uelewa na / au kufuata hatua za usimamizi wa hatari za usalama;
- ukosefu wa uwazi kuhusu wajibu na majukumu;
- ukosefu wa uwazi kuhusu hatua zilizochukuliwa na wasimamiaji;
- urithi wa ufuatiliaji duni kuhusu madai;
- ukosefu wa mafunzo na uhamasishaji kwa wafanyakazi;
- ukosefu wa ofisi ya maadili / mtetezi wa watu au ukosefu wa ulinzi wa mfichua uhalifu;
- ukosefu wa uwajibikaji na/au hatua kwa uongozi kufuatia madai;
- muundo wa mbovu wa uongozi; na
- kimya kikuu kuhusu ukatili wa kijinsia.

Shirika pia linashauriwa kuzuia masuala ya ndani ya kiutamaduni yanayoibua


hatari ya ukatili wa kijinsia, kama vile:

- kutokuwepo kwa usawa, ikiwemo kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia na ubaguzi dhidi ya wasifu tofauti;
- kukubalika kwa habari potofu za ubakaji (kama vile 'wanaume wote wanafanya hivyo');
- kuchukia wanawake;
- desturi ya kitabaka;
- uwepo wa washirika wa wahalifu (wa kiume na wa kike);
- matumizi ya dawa za kulevya (kama vile matumizi ya pombe kupita kiasi);
- uongozi mbaya;
- upendeleo na mtu fulani au kikundi cha watu na wasimamizi, ambao unaoweza kuathiri ikiwa tuhuma zitachukuliwa kwa uzito ikiwa tuhuma hizo zinahusu mtu huyo au kikundi hiki; na
- kukubali aina nyingine za utovu wa nidhamu, kama vile unyanyasaji wa kisaikolojia na ukandamizaji.

## 1.2. Jinsi ya kuzuia ukatili wa kijinsia

Mashirika mengi yana sera ya kutovumilia kabisa aina zote za ukatili wa kijinsia, ikijumuisha unyanyasaji wa kijinsia. Sera kama hizo zinaakisi uelewa kwamba mazingira ambayo unyanyasaji wa kijinsia haushughulikiwi yanaweza kusababisha mazingira ambayo yanafaa kwa makosa makubwa zaidi, kama vile
ubakaji na aina nyingine za shambulio. Kwa madhumuni ya kuzuia, aina tofauti za ukatili wa kijinsia zinapaswa kuonekana kama zinazohusiana na kuunda mwendelezo wa tabia (tazama Kielelezo cha 2).

Kielelezo cha 2: Piramidi ya unyanyasaji wa kijinsia




Imechukuliwa kutoka kwa Piramidi ya Vurugu na CCASA

Kwa kushindwa kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia na maoni ya kukera na utani, shirika linaweza kukubali mazingira ambapo uhasama wa kijinsia ni kawaida. Katika mazingira kama hayo, visa vidogo vinaweza kuongezeka na kuwa tabia mbaya zaidi ya ngono, kama vile kudhulumiwa mtandaoni,kuguswa bila kukubali na ubakaji. Unyanyasaji zaidi wa kijinsia au mwenendo mwingine usiofaa hufanyika katika shirika, kubwa zaidi ukiwa uwezekano wa visa vikubwa zaidi vya ukatili wa kijinsia.

Kwa hivyo, kama sehemu ya juhudi zao za kuzuia, mashirika yanapaswa kulenga kushughulikia visa vidogo kama vile vikubwa.

Ili kuzuia matukio ya ukatili wa kijinsia, timu za uongozi zinapaswa kulenga kuimarisha muundo wa shirika lao, michakato na mifumo. Jitihada za kuzuia visa vya ukatili wa kijinsia zina uwezekano mkubwa wa kuwa na ufanisi ikiwa shirika lina:

- uongozi wa wazi na msimamo thabiti kuhusu ukatili wa kijinsia;
- sera thabiti na wazi ya shirika;
- utekelezaji thabiti wa hatua za usimamizi wa hatari za usalama;
- mfumo jumuishi wa usimamizi wa hatari ya usalama, unaojumuisha kufanya tathmini jumuishi ya hatari;
- mikakati wazi na sawazishi ya kupiga ripoti kuhusu kero na visa, ikijumuisha muda wa kuchukua hatua kufuatia kupigwa kwa ripoti;
- mafunzo na uelekezi kwa wafanyakazi wote ili kuwahamasisha kuhusu hatari ya ukatili wa kijinsia na mikakati ya kupiga ripoti;
- mchakato wa uchunguzi huru;
- kanuni za maadili ya shirika;
- michakato wazi na unaofaa wa kutoa majibu unaolenga mnusurika;
- njia zisizo rasmi za kupiga ripoti ya visa zisizotegemea uchunguzi wa wasimamizi wakuu (unaoweza kuwa na upendeleo);
- mratibu wa maadili, mratibu wa kulinda usalama au mtetezi wa watu;
- ugavi ulio wazi baina muundo wa ngazi za mamlaka na wasimamizi wa malalamishi;
- uwajibikaji wazi; na
- usaidizi na mikakati ya ulinzi ambazo zinawasaidia manusura au wengine ambao wangetaka kuzungumza kuhusu makosa, kama vile sera ya ufichuzi wa uhalifu.


### 1.2.1. Tathmini jumuishi ya hatari

Masuala ya hatari ya kibinafsi na nje ya shirika ya ukatili wa kijinsia yanapaswa kujumuishwa katika mchakato wa tathmini ya kiwango cha hatari

ya shirika.

Tathmini ya hatari inapaswa kuzingatia vitisho vya nje na vya ndani, kama vile maingiliano yao (tazama Mchoro 3).

**Kielelezo 3:** Vitisho vya ndani na nje vinavyohusiana na utambulisho




Imenakilishwa kutoka EISF 'Kusimamia Usalama wa Wafanyakazi wa Misaada wenye Wasifu Mbalimbali

Utambulisho wa kijamii wa mtu una athari kwa mtu huyo kuhusu hatari ya ukatili wa kijinsia. Uchanganuzi wa tishio na uwezekano wa kuathiriwa lazima uzingatie jinsi wasifu fulani wa kibinafsi unavyoweza kuwa katika hatari kubwa zaidi kuliko wengine katika muktadha inayothathminiwa. Wakati mwingine ni mtazamo wa wasifu wa mtu binafsi badala ya wasifu halisi unaomweka mtu hatarini.

Kwa hatari za ukatili wa kijinsia, waratibu wa kulinda usalama lazima watatumie mtazamo wa utambulisho wa kijamii ili kuelewa jinsi mamlaka yanavyobadilikakuhusiana nawafanya kazi utambulisho wa kibinafsi na wajibu wa, shirika wa kutambua hatari zinazoweza kuwakumba kwa sababu hiyo.